

Ushairi - Kiswahili Notes

- [Istilahi za Kishairi](#)
- [Aina za Mashairi](#)
 - [Mashairi ya Arudhi](#)
 - [Mashairi Huru](#)
- [Ulinganishaji wa Shairi la Arudhi na Shairi Huru](#)
 - [Kufananisha](#)
 - [Kutofautisha](#)

[Istilahi za Kishairi](#)

1. Arudhi

- Sheria za jadi zinazofuatwa na watunzi wa mashairi:
 - kugawa shairi katika beti
 - beti kugawika katika mishororo inayolingana kiidadi
 - mishororo kugawika katika vipande
 - mishororo kuwa na mizani zinazolingana kiidadi (urari wa mizani)
 - kuwa na vina vya kati na vya mwisho vinavyotamkika kwa namna sawa (urari wa vina)
 - mtoshelezo wa beti au beti kutoa wazo kamili

2. Bahari

- Aina tofauti tofauti za mashairi k.m. ukara

3. Ubeti/beti

- Kifungu katika shairi kinachojitosheleza kimaaa

4. Mshororo

- Mstari katika ubeti

5. Mwanzo

- Mshororo katika ubeti

6. Mloto

- Mshororo wa pili katika ubeti

7. Mleo

- mshororo wa tatu katika ubeti

8. Kimalizio

- Mshororo wa mwisho ambao haurudiwi katika kila ubeti

9. Kibwagizo/mkarara/kipokeo/kiitikio

- Mshororo wa mwisho ambao hurudiwarudiwa katika kila ubeti na hubeba maudhui au kiini cha shairi.

10. Kipande/mgao

- Sehemu katika mshororo ambayo huonyeshwa na koma na huwa na kina

11. Ukwapi

- Kipande cha kwanza katika mshororo

12. Utao

- Kipande cha pili katika mshororo

13. Mwandamizi

- Kipande cha tatu katika mshororo

14. Mizani

- Silabi zinazotamkika katika mishororo

15. Urari wa mizani

- Kuwepo kwa idadi sawa ya mizani katika mishororo

16. Kina/vina

- Silabi zinazotamkika kwa namna sawa zinazopatikana katikati na mwishoni mwa sentensi.

17. Urari wa vina/vue

- Kuwepo kwa silabi zinazotamkika kwa namna sawa

[Aina za Mashairi](#)

1. Mashairi ya arudhi/Ushairi wa kijadi
 - Ambayo huzingatia sheria za jadi za utunzi wa mashairi.
2. Mashairi huru
 - Ambayo hayazingatii sheria za jadi za utunzi wa mashairi.

[Mashairi ya Arudhi](#)

1. Aina
 - tathmina (mshororo mmoja katika kila ubeti)
 - tathnia (miwili)
 - tathlitha (mitatu)
 - tarbia (minne)
 - takhmisa (mitano)
 - tasdisa (sita)
 - ushuri (kumi)
2. Bahari
 - mtiririko (mfanano wa vina vya kati na vya mwisho katika shairi zima)
 - ukara (vina vya mwisho kufanana na vya kati kutofautiana)
 - ukaraguni (vina vya kati na vya mwisho kutofautiana katika shairi zima)
 - kikwamba (mishororo kuanza kwa neno fulani katika shairi zima)